PRESS RELEASE
ISSUED BY INFORMATION SERVICES DIVISION
MINISTRY OF INFORMATION AND TOURISM
P. O. BOX 9142 DAR ES SALAAM TELEPHONE 20656

T
TIS
S

UNIV. COLL. DAR ES SALAAM LIBRARY

A/92/67
IT/I. 323

JANUARI 18, 1967
(11.00 A.M.)

# RAIS NYERERE ATOA RAMBIRAMBI KWA KIFO CHA CHIFU MAZENGO

Rais, Mwalimu Julius K. Nyerere ambaye yuno katika ziara ya mkoa wa Tabora leo (Januari 18) ametoa rambi rambi kwa ajili ya msiba wa kifo cha Chifu David Solomon Mazengo wa Ugogo kilichotokea jana huko Mvumi, Dodoma, kwa ndugu na jamaa za marehemu pamoja na wananchi wote wa Ugogo. Kifo hicho kilisababishwa na ugonjwa wa kukohoa na maumivu ya sikio.

Mwalimu Nyerere, ilielezwa kwamba alishtushwa na kusikitishwa sana na tukio hilo. Hivi sasa Rais amemwamuru Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Bwana John Mwakangale amwakilishe kwenye mazishi ya marehemu huyo yatakayofanyika huko Mvumi, leo hii.

Marehemu Chifu Mazengo alizaliwa mwaka 1860 huko Dodoma na alitawazwa kuwa Chifu mwaka 1904 baada ya kifo cha baba yake Chifu Chalula.

Marehemu huyo inasemekana alikuwa mojawapo wa Watemi maarufu sana nchini Tanganyika na kipenzi mkubwa wa Tanu. Mwaka 1962 wakati Tanganyika ilipojipatia Jamhuri, Chifu Mazengo alikuwa mmojawapo wa Wazee wawili waliomtawaza Mwalimu Nyerere kama Rais wa kwanza wa Tanganyika.

Marehemu alibatizwa mwezi Mei mwaka 1965 na kupewa jina la Solomon ambalo alimchagulia Rais Nyerere. Chifu Mazengo amewaacha wake sita, watoto 50 na wajukuu na vilembwekeze kama 200.

- mwisho -